

Spika wa Bunge, Dk Tulia Ackson akizungumza na wajumbe wa kamati teule ya Rais ya kutathmini ufanisi na utendaji wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki wakiongozwa na Mwenyekiti, Balozi mstaafu, Hassan Yahya (kulia kwake) walipomtembelea bungeni, Dodoma jana. (Picha na Ofisi ya Bunge).

HABARI LED UK 3.

Tanzania yataka nguvu uvuvi ukuze uchumi EAC

Na Mwandishi Maalumu,
Kampala

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, David Silinde amezisihi nchi wanachama wa Taasisi ya Uvuvi ya Ziwa Victoria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuungana na mamlaka zinazoshughulikia viwanda, biashara na takwimu kuhakikisha mchangwo wa sekta ya uvuvi unaonekana wazi kwenye Pato la Taifa la kila nchi.

Silinde alitoa wito huo jijini

Kampala, Uganda alipofungua Mkutano wa Tano wa Baraza la Mawaziri la Sekta ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji wa Taasisi ya Uvuvi ya Ziwa Victoria (LVFO) ya Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika juzi jijini humo.

Alisema suala la mchangwo wa sekta ndogo ya uvuvi kuonekana mdogo linatokana na ukweli kwamba mazao ya uvuvi yanahesabiwa katika sekta za kilimo na uzalishaji na mazao mengine yakiingizwa katika mnyororo wa

thamani wa sekta nyingine.

Akizungumzia ulinzi wa rasilimali za uvuvi katika Ziwa Victoria, Silinde alisema uvuvi haramu na uvuvi uliopitiliza unaohatarisha uwepo endelevu wa rasilimali za uvuvi na mazilia yake katika Ziwa Victoria na hivyo suala la ulinzi wake lazima litiliwe mkazo.

Alisema taarifa zinasema kuwa idadi ya samaki aina ya sangara kwa mfano imepungua kwa asilimia 33 katika muda wa mwaka 2021 na 2022 na

kuongeza kuwa nchi wana-chama wa LVFO haziwezi kukaa pembeni na kuacha vitendo hivyo vikiendelea kwa kuwa vinaathiri mamilioni ya watu ambao maisha yao yanategemea ziwa hilo.

Katika Mkutano huo Tanzania ilikabidhi kijiti cha uenyekiti kwa Uganda na kuipongeza kwa kuchukua nafasi hiyo na hivyo kuitakia utekelezaji mwema wa majukumu yake ya kulinda rasilimali za uvuvi katika Ziwa Victoria.

*Wafugaji waomba fidia kupisha mradi umwagiliaji

**Mradi mkubwa wa
kilimo cha umwagiliaji
unajengwa katika kitongoji
cha Mkalama, Kijiji cha
Kongogo wilayani hapa kwa
gharama ya Sh5.6 billioni na
mkandarasi wa Kampuni ya
CRJE kutoka China chini ya
Wizara ya Kilimo.**

Habel Chidawali, Mwananchi
hchidawali@mwananchi.co.tz

Bahi. Serikali imeruhusu kazi ya kujenga miundombinu katika mradi wa kilimo cha umwagiliaji iendelee, licha kutowekwa utaratibu wa mahali wafugaji wanakotakiwa kupeleka mifugo yao.

Juzi Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Godwin Gondwe, Mbunge wa Bahi, Kenneth Nolo na Mkuurugenzi Athuman Masasi na watalamu wa tume ya umwagiliaji, walikwenda kijijini hapo kuzungumza na wananchi baada ya kuibuka mvutano juu ya wapi watakwenda wakazi 760 wa kitongoji cha Mkalama amba-cho eneo lake limechukuliwa na mradi.

Kilio kikubwa kwa wananchi hao kilikuwa kuhusu wapi watakwenda ikiwa maeneo yao yanachukuliwa na mradi huo.

Hata hivyo, Gondwe aliwatoa hofu wakulima hao kwa kusema kuwa hakuna atakayenyang'anywa shamba lake, bali yataboreshwa.

Aliwataka wakazi wa kijiji hicho kuacha kukataa mradi wa



**"Bwawa linalojengwa siyo kwa
wageni tu, bali kipaumbele
cha kwanza kitakuwa kwa
waliookutwa ndani ambao
mashamba yao yataboreshwa
kwenye kilimo cha mpunga,"**
Godwin Gondwe

mabilioni ambao unakwenda kubadilisha maisha ya watu na bahati kwa okupata kwanikuna maeneo mengine wanaulilia. "Ondoeni mashaka, hakuna mtu atakayehamishwa eneo hili, bali mtakuwa wanufaika wa kwanza, kuhusu wafugaji mnawenza kuandika barua kuomba maeneo mengine mkipenda, lakini ndani ya mradi kutakuwa na matoleo ya maji kwa ajili ya milambo ya kunyweshea mifugo," alisema Gondwe.

Kwa upande wa mkazi wa Mkalama, Ngonongo Sanning'o alisema itakuwa ngumu kuvusha mifugo bila kugusa mashamba, hivyo akaomba Serikali kuwatafutia maeneo ya kwenda. "Mradi hatukatai, ila tunahoji ni maeneo yapi tutachunga kama kutakuwa na mashamba, tunaomba Serikali itusaidie kupata maeneo mengine au mtulipe fidia kidogo tuondoke," alisema Sanning'o.

Kwa upande wa Nolo alisisitiza kuwa katika eneo hilo hukutakuwa na kumhamisha mtu kwenda sehemu nyingine.